

## Grade 4 mid term 1 August 2021

### Kiswahili

#### ZOEZI LA 1: KUSOMA KWA UFAHAMU.

- i) Soma hadithi hii kisha ujibu maswali.

Alhamisi yenyewe, tulikuwa tumetutia darasani kimya huku tukifanya mtihani wa katikati ya muhula. Punde si punde, tuliona wingu la moshi upande wa jikoni. Kila mmoja wetu akatoka mbio ili tukaone kilichokuwa kikiendelea. Tulisukumana kwa sababu kila mmoja alitaka kufika wa kwanza. Wengine wetu walianguka na kuumia vibaya. Kufika, moto ulikuwa umevichoma vyombo na vyakula. Ulikuwa mkubwa zaidi, ukapanda hadi paani. Tulipiga kamsa ili kuwaita majirani lakini moto huo ultuzidi nguvu sote.

1. Mkasa wa moto ulitokea siku ya \_\_\_\_\_
2. Wanafunzi walitulia darasani wakifanya mtihani wa \_\_\_\_\_
3. Wingu la moshi lilionekana upande wa \_\_\_\_\_
4. Watoto hao walisukumana kwa sababu \_\_\_\_\_
  
5. Moto huo mkubwa ulikuwa umechoma \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_

- ii)

Wanyama wafugwao nyumbani huitwa wanyamahowa. Wengi wao hutupa vitu mbalimbali kama vile maziwa, nyama, mayai, ngozi na mbolea. Hata hivyo, kuna wengine ambao huwa mapambo tu. Paka, licha ya kuwa pambo, hutusaidia kuwanasa panya ambao huwa waharibifu sana. Paka ni mnyama safi sana. Yeye hupenda kujilaza kwenye makochi laini akilala.

Mbwa ni pambo na pia husaidia kuyalinda maskani yetu dhidi ya wezi na watu wengine wabaya. Hata hivyo, kuna aina fulani za mbwa ambao hawawezi kutulinda. Wao huwa mapambo tu ya nyumbani.

6. Wanyamahowa ni \_\_\_\_\_
7. Wanyamahowa huweza kutupa \_\_\_\_\_
8. \_\_\_\_\_ ni wanyama waharibifu,
9. \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_ huwa mapambo ya maskani yetu.
10. Tumeambiwa kuwa mnyama safi sana ni \_\_\_\_\_

## ZOEZI LA 2: SARUFI

Chagua neno sahihi kujazia pingo.

wazazi	Mungu	mchwa	heshima	walimpeleka
--------	-------	-------	---------	-------------

Pendo alikuwa msichana mwenye bidii ya \_\_\_\_\_ . Pia, alikuwa mtoto

11

mtiifu kwa wote. \_\_\_\_\_ wake walimlea kwa \_\_\_\_\_ ya hali ya juu.

12

13

Walimfunza kuwasalimia wakuu kwa nidhamu. Vilevile, \_\_\_\_\_ kanisani

14

kujifunza jinsi ya kumwomba \_\_\_\_\_. Kila mtu kijijini alimpenda Pendo.

15

## ZOEZI LA 2: SARUFI

Pigia misitari nomino katika sentensi hizi.

16. Kiti chako kilinunuliwa na nani?

17. Hii ndiyo nyumba ilijoengwa vizuri.

18. Hawa ndio ng'ombe walioletwa jana.

Andika katika umoja au wingi.

19. Mjomba anatembea polepole.

20. Sungura wamelala pale.

21. Mdudu alitambaa akaenda.

Linganisha aina za maneno.

22. Lakini Kivumishi

23. Chora Kielezi

24. Chafu Kiunganishi

25. Haraka Kitenzi

### **ZOEZI LA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

*Mwalimu amwamkue mwanafunzi na kumwomba acae. Mwalimu ajitambulische.*

*"Mimi ni mwalimu \_\_\_\_\_ Niambie jina lako."*

*"Leo ningependa tuzungumze kuhusu nyumbani."*

1. Baadhi ya vyombo vinavyoweza kupatikana jikoni ni gani?
2. Magodoro, vitanda na mablanketi hupatikana katika chumba kipi?
3. Chumba cha kuogea huitwaje?
4. Sebule ni chumba cha kufanya nini?
5. Watu huenda haja kubwa na ndogo katika chumba gani?

Alama
5

### **ZOEZI LA 2: KUSOMA KWA SAUTI.**

Kiamshakinywa ni chakula cha kwanza kabisa katika siku. Mara nyingi, chakula hiki huliwa asubuhi. Hiki ndicho chakula muhimu kuliko chamcha na chajio. Tukila chakula bora asubuhi, miili yetu huwa tayari kwa shughuli nyingi za siku. Watu wengi huamini kuwa chakula cha asubuhi, yaani kiamshakinywa, lazima kiwe chai. Huu si ukweli.

Alama
10